

nini maana ya haya maneno aliyosema Bwana ; Tuliwapiga filimbi
wala hamkucheza; Tuliomboleza wala hamkulia?

SWALI 1:Bwana Yesu aliposema huu mfano alikuwa anamaanisha nini?..

“Lakini nitakifananisha na nini kizazi hiki? Kimefanana na WATOTO wanaokaa SOKONI,WANAOWAITA wenzao,wasisema,Tuliwapigia FILIMBI,wala hamkucheza; TULIOMBOLEZA,wala hamkulia.MAANA YOHANA ALIKUJA,HALI WALA HANYWI,WAKASEMA,YUNA PEPO.MWANA WA ADAMU ALIKUJA,AKILA NA KUNYWA,WAKASEMA,MLAFI HUYU,NA MLEVI,RAFIKI YAO WATOZA USHURU NA WENYE DHAMBI!” NA HEKIMA IMEJULIKANA KUWA INA HAKI KWA KAZI ZAKE”.(Mathayo 11:16-19).

JIBU: Mfano huo ni sawa ni kizazi cha sasa hivi tulichopo tuchukulie tu mfano, Mtu akitokea ni mtumishi wa Mungu kweli, maisha yake yote ameyachagua ni kukaa tu kanisani, au milimani kuomba, hafanyi kazi yoyote isipokuwa ni kuomba tu, na kuhudumu kanisani, hana pesa nyingi, nguo zake sio mpya sana, hana mke, wala marafiki, yeye kazi yake ni kumtumikia tu Mungu basi, kajikana maisha yake yote hataki chochote isipokuwa Mungu kajizuia kila kitu kwa ajili ya ufalme wa mbinguni ..Unadhani watu huku nyuma watamchukuliaje mtu kama huyo??..Si ajabu watamwita mlokole masalia, au kalogwa, watasema Mungu hayupo hivyo, Mungu anataka watumishi wake wawe na maisha

nini maana ya haya maneno aliyosema Bwana ; Tuliwapiga filimbi
wala hamkucheza; Tuliomboleza wala hamkulia?

ya kujifurahisha, kama vile Sulemani, na sio kuwa kama vichaa wa barabarani wasiokuwa na malengo..watamwambia hakika wewe utakuwa umeingiliwa na roho nyingine ambayo si ya Mungu....hivyo hatutaweza kukusikiliza mtu kama wewe maskini wa roho na kimawazo...sisi tunawasikiliza wahubiri wenyewe malengo, na mafanikio.

Lakini watu hao hao, mfano wakimuona mtumishi wa Mungu kweli labda Mungu kampaka mafuta anahubiri Neno na Mungu katika kweli yote, kambariki na maisha mazuri ya duniani, labda kampa nyumba nzuri, nguo nzuri, kampa familia nzuri, kampa mali nyingi, analo kanisa kubwa, ..utashangaa watasema, watumishi wa Mungu huwa hawapo hivyo, watumishi wa Mungu hawawezi wakawa matajiri, huwa wanakaa tu milimani wanautafuta uso wa Mungu usiku na mchana, na sio kwenye majumba ya kifahari kama watu wa mataifa.....Kwahiyo kwao pia watasema hatuwezi kuwasikiliza nyie matapeli mnakula Fedha za waumini..

Na ndivyo ilivyokuwa katika mfano huo, Mungu alipojaribu kuwapeleka Israeli nabii aliyejikana kwa kila jambo, (Yohana mbatizaji) wakasema mtu wa kawaida hawezi kuishi maisha kama hayo ya kutokula wala kujichanganya na wengine, ni lazima atakuwa anao pepo, Lakini Bwana alipokuja anakula na kunywa pengine akidhani kuwa labda watamsikia na yeye wakamwambia ni mlafi na mlevi, manabii wa Mungu hawawi

nini maana ya haya maneno aliyosema Bwana ; Tuliwapiga filimbi
wala hamkucheza; Tuliomboleza wala hamkulia?

hivyo.....Ndio mithali hiyo inakuja, walipopigiwa filimbi ili wacheze
wakakataa, pengine wanahitaji maombolezo, lakini pia
walipoombolezewa hawakulia,..sasa waelewekeje! Kwenye raha hawapo
kwenye huzuni hawapo..Na ndivyo ilivyo katika kizazi hiki..hata kipewe
ishara gani ya nabii hakitaamini isipokuwa wale tu waliokusudiwa tangu
kuwekwa misingi ya ulimwengu ndio watakaoamini ..

Ubarikiwe!

Mada zinazoendana:

**BWANA ALIMAANISHA NINI KUSEMA HAKUNA MTU ASHONAYE
KIRAKA CHA NGUO MPYA KATIKA VAZI KUKUU?**

WATU WASIOJIZUIA.

TUJIFUNZE JAMBO KWA WANAWAKE HAWA WAWILI:

**SHETANI ANATOLEA WAPI FEDHA, ANGALI TUNAJUA FEDHA
NA DHAHABU NI MALI YA BWANA?**

nini maana ya haya maneno aliyosema Bwana ; Tuliwapiga filimbi
wala hamkucheza; Tuliomboleza wala hamkulia?

HUYU AZAZELI NI NANI TUNAYEMSOMA KATIKA(WALAWI 16:8)

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp